TANGAZO LA SERIKALI Na. 48 la tarehe 24/1/2025

SHERIA YA HIFADHI ZA JAMII,
(SURA YA 135)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 38)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MATUMIZI YA MAFAO YA MWANACHAMA KAMA DHAMANA YA MKOPO WA NYUMBA ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 149 la 2024

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Matumizi ya Mafao ya Mwanachama kama Dhamana ya Mkopo wa Nyumba za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Matumizi ya Mafao ya Mwanachama kama Dhamana ya Mkopo wa Nyumba za Mwaka 2025 ambazo katika Kanuni hizi zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 13

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 13 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo mpya zifuatazo:

"(3) Mgogoro chini ya kanuni hii utawasilishwa kwa maandishi kwa msuluhishi ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ambayo mgogoro umetokea ukielezea kwa ufupi kiini cha mgogoro.

(4) Msuluhishi, ndani ya siku saba baada ya kupokea mgogoro, atawataarifu wahusika mahali, tarehe na muda wa kufanya usuluhishi ambao hautakuwa zaidi ya siku ishirini na moja kuanzia tarehe ya kupokea mgogoro.

(5) Usuluhishi unaweza kufanywa katika kikao kimoja au zaidi isipokuwa katika mazingira yoyote kipindi cha usuluhishi hakitazidi muda wa siku thelathini kuanzia tarehe ya kikao cha kwanza cha usuluhishi.

(6) Wakati wa usuluhishi, wahusika wanaweza kubadilishana nyaraka muhimu ambazo zinaelezea kiini cha mgogoro, misimamo na maslahi ya wahusika.

(7) Msuluhishi atafanya usuluhishi kwa uhuru na bila upendeleo na atawezesha mawasiliano baina ya au miongoni mwa wahusika kwa ajili ya kuwasaidia kufikia muafaka unaokubalika na pande zote.

(8) Endapo makubaliano yanafikiwa katika mgogoro, wahusika watasaini makubaliano ya muafaka.

(9) Endapo makubaliano hayatafikiwa katika mgogoro, wahusika wanaweza kutumia njia nyingine zilizopo kwa mujibu wa sheria husika.”.

Dodoma,
20 January, 2025

RIDHIWANI J. KIKWETE,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya WaziriMkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*